



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU RUFAA YA MGOMBEA KITI CHA
UDIWANI KATA YA NDEMBEZI KUPITIA CHAMA CHA ACT WAZALENDO
DHIDI YA MSIMAMIZI WA UCHAGUZI JIMBO LA SHINYANGA MJINI**

Dodoma, 25 Septemba, 2021

Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika kikao chake cha tarehe 24 Septemba, 2021, ilijadili na kutoa uamuzi kuhusu rufaa iliyowasilishwa na Ndugu Mvano Abdul Iddy – Mgombea Udiwani katika Kata ya Ndembezi, Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga kupitia Chama cha ACT Wazalendo dhidi ya Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Shinyanga Mjini. Katika rufaa hiyo, Mrufani alikuwa akipinga uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Shinyanga Mjini kutengua uteuzi wake kutokana na pingamizi lililowekwa dhidi yake na Ndugu Victor Thobias Mmanywa - Mgombea Udiwani katika Kata ya Ndembezi kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM).

Baada ya kuipitia rufaa hiyo, Tume kwa mamlaka iliyonayo kwa mujibu wa kifungu cha 44(5) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 kikisomwa pamoja na kanuni ya 30 (3) ya Kanuni za Uchaguzi wa Madiwani za mwaka 2020 IMEKATAA rufaa hiyo na IMEKUBALIANA na uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi katika Kata ya Ndembezi wa kutengua uteuzi wake.

Uamuzi wa Tume umefikiwa baada ya kujiridhisha kwamba nyaraka zilizowasilishwa na Mrufani hazikuwa na uthibitisho wa kuonesha kuwa alitoa tamko la kuheshimu na kutekeleza Maadili ya Uchaguzi mbele ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kama inavyotakiwa na kanuni ya 24(6) ya Kanuni za Uchaguzi wa Madiwani za mwaka 2020, ikisomwa pamoja na kipengele cha 1.4 cha Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2020.

Imetolewa na:

Dkt. Wilson Mahera Charles

MKURUGENZI WA UCHAGUZI